raising children network
the australian parenting website

# Uleaji wa watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili: machaguo

Inafaa kwa
**0-18**
miaka

**https://raisingchildren.net.au/newborns/connecting-communicating/bilingualism-multilingualism/raising-bilingual-children-tips**

## Mambo makuu

- **Kuna mifano miwili ya uleaji wa watoto wanaozungumza lugha mbili au lugha nyingi – mtu mmoja-lugha moja, na lugha ya tamaduni kama lugha ya nyumbani.**
- **Njia nzuri zaidi ya kuwasaidia watoto kusoma msamiati mkubwa katika lugha nyinginezo mbali na Kiingereza ni kuzungumza nao lugha hizi.**
- **Unaweza kusaidia uboreshaji wa lugha mbili au lugha nyingi anazozungumza mtoto wako, shughuli za kijamii na shughuli za kila siku pale nyumbani.**

## Kuhusu kulea watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili

Iwapo wewe na mwenzio wako mnazungumza lugha nyinginezo bali na Kiingereza, unaweza kutaka watoto wako kukua wakijua lugha hizi. Kulea watoto wanaozungumza lugha mbili au lugha nyingi kuna manufaa mengi. Kwa mfano, kunaweza kuboresha mawasiliano na mahusiano katika familia unayoishi nayo na katika watu wa ukoo.

Njia bora zaidi ya kuwasaidia watoto wako kusoma msamiati mwingi katika lugha nyinginezo isipokuwa Kiingereza ni kuhakikisha unatumia lugha hizi kila wakati na wao, hasa katika miaka yao ya utotoni.

## Uleaji wa watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili: chaguo za familia yako

Maamuzi ambayo wewe na mwenzio mtafanya kuhusu kuwasaidia watoto kusoma kutumia lugha zenu kunategemea hali ya familia yako.

### Mtu mmoja-lugha moja

Iwapo wewe na mwenzio mnazungumza lugha tofauti, **mfano wa mtu mmoja-lugha moja** kwa kusaidia uzungumzaji wa lugha nyingi au lugha mbili kunaweza kukufaa.

Kwa mfano, iwapo lugha yako ni Kiingereza na ya mwenzio ni Kimandarini, unaweza kuzungumza kwa Kiingereza na watoto wako na mwezio kuzungumza Kimandarini na wao.


© Raising Children Network

Mfano huu unaweza kufanya kazi na **lugha zaidi ya moja bali na Kiingereza**. Kwa mfano, iwapo unazungumza Kihispania na mwenzio anazungumza Kiitaliano, nyinyi wawili mnazungumza lugha zenu binafsi kwa watoto wenu mkiwa nyumbani. Iwapo nyinyi wawili mnazungumza Kiingereza, unaweza kuchagua kutumia Kiingereza na wao nje ya nyumbani. Watoto wako pia watasoma utumiaji wa lugha ya Kiingereza wakiwa shuleni na katika jamii.

Ni vizuri iwapo nyinyi wawili mnaelewa lugha zenu kwa hivyo hakuna mmoja wenu anahisi ameachwa nje mnapozungumza lugha ya kila mmoja kwa watoto wenu.

**Lugha ya urithi kama lugha ya nyumbani**
Iwapo wewe na mwenzio mnazungumza lugha ya urithi mkiwa wawili, unaweza kuifanya lugha hii kuwa mnayozungumza na familia yako mkiwa nyumbani.

Kwa mfano, unaweza kuwa ulihama kutoka Iraki hadi Australia na kuzungumza Kiarabu kwa watoto wenu mkiwa nyumbani. Kiarabu ndio lugha yenu ya urithi. Watoto wenu pia wanakwenda shuleni na kuzungumza Kiingereza na marafiki zao na walimu.

Mfano mwingine ni iwapo wewe na mwenzio mko na matatizo ya usikiaji na mnalea watoto wanaoskia. Watoto wako wanaweza kusoma Kiuslani wakiwa nyumbani, na Kiingereza katika jamii ya usikiaji.

Mfano wa lugha ya urithi unamaanisha kuwa watoto wako wanaweza kusikia, kuzungumza na kutumia lugha yenu ya urithi sana, kwa sababu kila mtu katika familia anaitumia.

> Watoto wanaweza kutotaka sana kuzungumza nawe kwa lugha nyingineyo isipokuwa Kiingereza wanapozeeka. Ni vizuri kuendelea kutumia lugha hii hata kama watoto wako wanapenda sana kujibu Kiingereza.

## Uleaji wa watoto wanaozungumza lugha nyingi au lugha mbili: vidokezo

Hapa kuna vidokezo vya utendaji vya kusaidia ukuaji wa mtoto wako wa lugha nyingi au lugha mbili.

### Uchezaji na michezo

- Soma na kuambiana hadithi katika lugha yako, na umhimize mtoto wako kushiriki. Tumieni mavazi na muwe wabunifu!
- Chezeni michezo kwa lugha yenu, hasa michezo inayozingatia lugha, kama vile ‘I spy’, bingo, ‘who am I?’ na kumbukumbu.
- Imbeni nyimbo, mcheze densi na kucheza mziki katika lugha yenu. Watoto wanapenda muziki, na melodia njia nzuri ya kuwasaidia kukumbuka mambo.
- Tafuta programu za michezo ya maneno katika lugha yenu ya urithi kwa ajili ya mtoto wako.

### Shughuli za kijamii


© Raising Children Network

- Tafuta shule, vituo vya utunzaji wa watoto na programu zinazotumia lugha mbili au nyingi ambazo zinasaidia mtoto wako kutumia lugha.
- Panga nyakati za michezo na watoto wengine ambao wanazungumza lugha kama yenu ya urithi.
- Panga ziara kwa au kutoka kwa wazungumzaji wa lugha yenu. Iwapo inawezekana kwako, kutembelea mataifa ambayo watu wanazungumza lugha yako kunaweza kuboresha uchu wa mtoto wako wa kutaka kujua utamaduni na uwezo wa kuzungumza lugha hii.
- Tembelea maktaba na kuomba diski za sauti, Diski za Video, vitabu vilivyochorwa picha, vitabu na majarida ya tamthiliya ya lugha yako yanayofaa kiumri.
- Tafuta shughuli za kitamaduni ambazo wewe na mtoto wako mnaweza kufanya pamoja ili kujijuza zaidi urithi wa utamaduni na utambulisho wenu. Kwa mfano, Siku ya Harmony kila mwezi wa Machi katika mwaka inasherehekewa kote katika Australia.

**Nyumbani**

- Sikizeni programu za redio katika lugha yenu, ikiwa ni pamoja na programu maarufu za muziki na vituo vya watoto.
- Iwapo una familia na marafiki ambao wanaoishi ng'ambo, unaweza kuwahimiza watoto wako kuungana nao kupitia programu ya ujumbe wa video au kupitia mtandao.
- Fikiria ni nini anachopenda mtoto wako – kwa mfano, mpira, muziki, vipindi vya runinga, mapishi na kadhalika. Jaribu kushirikisha lugha yako katika mambo haya anayoyapenda. Kwa mfano, unaweza kutafuta maelekezo ya mapishi anayoyapenda mtoto wako au maelekezo ya mapishi ya kawaida tu kutoka kwa jamii yako na kuyapika pamoja naye huku mkitumia lugha yenu tu.
- Tazameni filamu au spoti katika lugha yenu – kwa mfano, kupitia runinga ya setilaiti au huduma za utiririshaji kupitia mtandao. Unaweza mara nyingine kuwasha sauti na manukuu ya sauti ya maudhui ya Kiingereza katika lugha nyinginezo.
- Wasaidie watoto wako wakubwa au vijana kupata jamii salama za mtandaoni, zilizo na misingi wa mapendeleo. Zingatia usalama katika mtandao wa watoto wakubwa na usalama wa vijana katika intaneti.


© Raising Children Network